

## Captain Smyzy "Majuto"

Visit "[Majuto](#)" on MotoLyrics.com

....yeah, thiz about life man.....(chiness bizness) Every  
thing you do, Fikiria, hujui place utaishia...au sio  
verse 1

Skiza story yake, mwana wa mabepari  
toka alipozaliwa hali yake ilikuwa shwari  
kama mtoto ye yote aliishi na wazazi  
na alipotak chochote alitegemea wazazi  
hizo hela za babake zilimpa ujeuri  
hakuna mtu ye yote aloweza kumshauri  
wote aliwachukua tu kama watu mabwege  
bila kujua hatimaye hali yake itakuwaje  
wazazi walimpenda mshkaji kaanza kudeka  
kajiona ameshafaulu shuleni akatoweka  
kaijunga na vikundi haram wakamchombeza  
mi nashindwa kwani hakufaham watampoteza?  
mshkaji alizidisha vituko kila kukicha  
leo kaiba mbuzi kesh okuku kamficha  
kapelekwa kwa chief, ili apate kumkashif,  
hapo bado kaishia kumtongoza mke wa chifu.

Chorus

Nilimuonya lakini hakusikia  
aliona kama mimi siwezi kumsaidia  
cheki sasa hatimaye anajutia  
vitu alivofanya ndo sa' vinamchukia x2

verse 2

Zilipita siku chache hali ikizidi kuwa mbaya  
bwana chifu kampitisha kwenye koti za wilaya  
mateso aloyapata siwez kusimulia  
na mpaka siku ya leo bado nazifikiria  
alifanywa atembee huku amefungwa miguu  
wakamweka kwenye celi akisubiri siku kuu  
back at home, watu walishachoka naye  
mpaka wazazi wake walishachoka kuishi naye  
siku ilipowadia alipelekwa mahakamani  
kesi yake iliposikizwa alihukumiwa maishani  
cheki sasa anajuta, nafsi inamsuta  
kwani ye ye ndo chanzo kwa yale yote yalomkuta  
sina uwezo wowote mie wa kumsaidia  
nilimuonya mara mia kaniona kama gunia  
so, peace for life, namalizia story yangu  
asiyefunzwa na mama hufunzwa na ulimwengu.  
chorus x2

Visit [Captain Smyzy](#) page on MotoLyrics.com, to get more lyrics and videos.

---

[MotoLyrics.com](#) | Lyrics, music videos, artist biographies, releases and more.